

Virginia SUN Bucks



Mpango wa shirikisho ulioundwa kupambana na uhaba wa chakula kwa kuwapa watoto wanaostahiki **usaidizi wa chakula wa mara moja wa \$120** kupitia kadi ya Virginia SUN Bucks au kadi ya SNAP EBT wa kutumia kununua bidhaa za chakula.



Nani anastahiki moja kwa moja kupata Virginia SUN Bucks na hahitaji kutuma ombi?

Mtoto wako huandikishwa kiotomatiki kwenye Virginia SUN Bucks ikiwa:

- ✓ Anapokea usaidizi wa SNAP au TANF au anashiriki katika Medicaid inayolingana na mapato.
- ✓ Alituma ombi la, na kupokea milo ya bila malipo au ya bei iliyopunguza shuleni katika mwaka wa shule wa 2025–2026 kupitia **Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana Shuleni**.



Je, nitajuaje ikiwa familia yangu inahitaji kutuma ombi la Virginia SUN Bucks?

Ikiwa mtoto wako hakutuma ombi na hakupokea milo ya bila malipo au ya bei iliyopunguzwa shuleni kupitia Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana Shuleni na familia yako haishiriki katika SNAP, TANF au Medicaid inayolingana na mapato, ni lazima utume ombi.

Je, VDSS itatoa usaidizi wa Virginia SUN Bucks lini na vipi?

Usaidizi utatolewa **kuanzia Juni 2026 kwa mfululizo** kwa watoto wanaotimiza sifa zinazohitajika kiotomatiki na kwa familia zinazostahiki baada ya kutuma maombi. Usaidizi wa wapokeaji wa SNAP utawekwa kwenye kadi yao iliyopo ya SNAP EBT na wale wasiopokea SNAP watapokea kadi ya SUN Bucks itakayotumwa kwa posta kwenye anwani iliyo kwenye rekodi.

Ninawezaje kutuma ombi?

Unaweza kutembelea VirginiaSunBucks.com ili kutuma ombi mtandaoni au uchapishe na kutuma ombi kwa barua kwenye 5600 Cox Road, Glen Allen, VA 23060 kufikia tarehe 31 Agosti. Vinginevyo, unaweza kuwasilisha ombi kwa kupiga simu kwa Kituo cha Simu cha Virginia SUN Bucks (866-513-1414) kuanzia tarehe 15 Juni hadi tarehe 31 Agosti.



Unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu Virginia SUN Bucks kwenye VirginiaSunBucks.com.



VIRGINIA DEPARTMENT OF
SOCIAL SERVICES

**VIRGINIA
SUN
BUCKS**